# Table of Contents

HEKIMA NA MAARIFA YA KI-MUNGU KATIKA UCHUMI ........ 3

SOMO LA UJASILIAMALI........ 5

HISTORIA YA FEDHA. ........ 5

FAIDA ZA KUWA TAJIRI ........ 5

NAMNA YA KUWA TAJIRI ........ 6

Ujasiliamali ni nini?........ 7

KANUNI ZA UJASIRIAMALI ZA KI-MUNGU........ 8

Afya na Agano la Mungu ........ 8

Uwe na lugha nzuri ........ 8

TUMIA VIZURI ULIMI WAKO WEWE MTU WA MUNGU ........ 9

Tutazungumzia mambo gani matatu? ........ **Error! Bookmark not defined.**

Angalia wakati gani unapaswa kusema na nani unataka kusema naye,na ni kwa nini unataka kusema ........ 10

JAMBO LA KUSEMA ........ 12

JINSI YA KUSEMA........ 14

Uwe na moyo wa kufanya kazi........ 15

Muda........ 17

Mtandao ........ 17

Unawezaje kupata marafiki mzuri? Ni mambo gani yanayohitajika ili kupata marafiki wa kudumu? ... 19

**Kujali watu** ........ 19

Urafiki WA kweli unahusisha vitendo Na siyo Kwa maneno tu, rafiki mzuri anajua majukumu yake, na ni mwenye kujali. Ni vizuri uwe na urafiki unahusisha pande mbili, na kila mmoja anapaswa kutimiza sehemu ya mahitaji yake.(win win situation). Pia kuna faida za kufanya hivyo. Jiulize, 'Je, upo tayari kujitoa kutumia muda na mali zako kwa ajili ya rafiki yako?' Kumbuka, ili upate rafiki mzuri, *wewe* mwenyewe unapaswa kuwa rafiki mzuri. ........ 19

Msitengane wakati wa mafanikio........ 21

Njia Mbalimbali za Kupata Mafanikio........ 21

Uwe na Mawazo Yanayofaa Kuhusu Pesa........ 22

........ 22

Imarisha Roho ya Ukarimu ........ 22

Samehe kwa Hiari ........................................ 23
Ishi Kulingana na Viwango vya Mungu ........................................ 23
Onyesha Upendo Usio na Ubinafsi ........................................ 24
MAMBO YATAKAYOKUFANYA UPATE MAFANIKIO ZAIDI ........................................ 25
MFUMO WA BIASHARA ........................................ 28
IJUE BIASHARA YA MTANDAO (NETWORK MARKETING) NA FAIDA ZAKE. KONA YA MJASIRIAMALI NA EDMARK HEALTHY LIVING & FINANCIAL PROSPERITY ........................................ 29
FAIDA ZA BIASHARA MTANDAO ........................................ 30
. UHURU BINAFSI. ........................................ 31
FURSA KUBWA ZA MAFANIKIO ........................................ 31
KUFANYA BIASHARA UKIWA NYUMBANI/WORK AT HOME ........................................ 32
KUTOKUWA NA MIPAKA NA JINSI YA KUIENDESHA ........................................ 33
KUPATA MSHAHARA/KIPATO CHA ZIADA ........................................ 33
KUENDELEA KUPATA KAMISHENI HATA KAMA UTASIMAMA KWA MUDA KUSAMBAZA BIDHAA. ........................................ 34
KANUNI AMBAZO ZITAKUSAIDIA KUANZA NA KUKUZA BIASHARA YAKO KWA KUWA NA MTAJI MDOGO ........................................ 35
Jipe muda, biashara haitaweza kukua kwa haraka ........................................ 35
3. Angalia gharama za matumizi yako ........................................ 37
4. Chagua marafiki ........................................ 37
Biblia inasema nini kuhusu Mkristo kuingia katika madeni? Ni makosa kukopa au kukopesha pesa?" .... 39
Wale ambao wameshindwa kuwalipa, lakini haiwahukumu wenye deni. ........................................ 39
HEKIMA YA KI-MUNGU KATIAK MAFANIKIO ........................................ 41
SIFA ZA MFANYABIASHARA: ........................................ 42
MAMBO YA KUZINGATIA: ........................................ 42
NAMNA YA KUTAMBUA WATEJA: ........................................ 43
UWEZO WA KUSIMAMIA BIASHARA: ........................................ 43
MANUFAA YA KUFAHAMU GHARAMA ZA BIASHARA: ........................................ 44
MAKATAZO: ........................................ 45

# HEKIMA NA MAARIFA YA KI-MUNGU KATIKA UCHUMI

## *(ANZA SASA UTAJIRIKE*)

Hekima ya kweli ni uwezo wa kutenda ifaavyo kulingana na ujuzi na uelewa.Hekima ni kinyume kabisa cha upumbavu, ujinga na ukichaa. Katika kitabu cha methali kimezungumzia sana kuhusiana na hekima hekima hekima hivyo basi ukitaka kupata ujuzi wa hekima na maarifa yanayofaa basi ni vizuri uendelee kusoma kitabu cha methali (methali 4:7)

Mungu anakupatia hekima Kwa kukukirimia kipimo cha uwezo na ujuzi wake wote. Hekima na maarifa tunayopata kutoka kwa Mungu tukiitumia vizuri pasipo kupofushwa katika akili kutoka kwa adui shetani tutafanikiwa kuwa katika uchumi timilifu (Efeso 1:8).

Mungu alivyomuumba mwanadamu ni mpango wake madhubuti kiumbe hiki kifanikiwe katika maisha, kifanikiwe katika fedha, katika afya na katika Kiroho.

Bwana akanena na Musa na kumwambia angalia nimemwita kwa jina lake Bazaleli mwana wa Uri, mwana wa Uri wa kabila la Yuda, nami nimemjaza Roho ya Mungu katika Hekima na Maarifa na Ujuzi na mambo ya kazi ya kila aina ili abuni kazi za ustadi kuwa fundi wa dhahabu na wa fedha na wa shaba na kukata vito kwa kutiwa mahali na kuchora miti na kufanya kazi za ustadi iwayo yote (kutoka 31:1-5). Tumeona wazi kuwa hatupaswi kuchagua kazi haijalishi una elimu au hauna elimu bali kazi yoyote unaweza kuifanya mfano mtaani kwako kuna shida ya maji tambua hiyo ni fursa unatakiwa utafute namna ya kuuza maji katika eneo hilo, au unaona hapo mtaani kuna uhaba wa kitu Fulani kama magenge, hata kama kuna magenge unaweza kuwa na la kwako na ukawa mbunifu mfano vitu hivyohivyo vinavyopatina kwenye magenge mengine wewe unaviboresha mfano unauza dagaa wewe unatoa vichwa, unauza mbogambonga basi wewe unaosha na kukatakata kwa kufanya hivyo utawavutia wateja kwa wingi na utauza kuliko wengine hiyo ndiyo fursa kwani tambua hata mbuyu ulianza kama mchicha. Usipende kwenda juu kabla haujaanzia chini, biblia inasema katika atakaekuwa muaminifu kwa vichache atakuwa muaminifu kwa vikubwa pia.

RAYMOND CHIMBUYA

Shetani liye baba wa uwongo amepovusha fikra za baadhi ya wanadamu ili waweze kuhisi Utajiri ni wa shetani. Mwana wa Mungu haupaswi kuwa tajiri. La hasha, hata wamejaribu kutafsiri maandikoko kiupotofu ili kutetea hoja ya umaskini kwa Mwana wa Mungu.Hekima na Maarifa leo yakufunguwe kwa Jina la Yesu.

Ni mpango wa shetani kuua na kuaribu maisha ya mwanadamu,kumbuka fedha katika historia yake ni Mbinguni.Shetani alianza kumjaribu Bwana Yesu kule mlimani ili aweze kumpa fahari za nchi na umiliki katika utawala wake.Kumbuka Yesu Kristo alivyomjibu,alimwambia ‘’USIMJSRIBU BWANA MUNGU WAKO’’.Anachotaka kujaribu shetani hapa ni kuondoa haki yake kisha amrejeshee haki yake na ajifanye yeye ndiye kampa hiyo haki yake.Mungu alivyomuumba mwanadamu alimpa uwezo wa Kutawala kila kitu,atawale wanyama ,fedha, ndege kila kilichopo duniani.Baada ya wivu wa shetani akakengeuka na kumwasi Mungu,kisha akatupwa nche ya uso wa dunia ndipo akawa mfalme wa dunia hii.

Mapambano yanaendelea katika yake na wana wa Mungu,ukitata kupata fedha pasipo kutumia kanuni ya Mungu ,utapata shariti ni moja kumsujudia yeye aliye mwovu atakupatia fedha ili ufurahiye kwa muda maalumu na heshima ya muda kisha uingiye motoni milele na umfanyiye kazi zake.

Shetani anageuza kanuni ya Mungu yamafanikio, anataka utowe kafara na mambo maovu yanayofanana na jina lake na uthihirisho wa matendo yake. Kwa mfano,ukitaka kupata fedha kwa njia ambayo ni nje na kanuni za Ki-Mungu,mtumikiye shetani utazipata,kujiunga na shetani ni rahisi kutoka ni ngumu.Mungu anataka ufanikiwe katika Nyanja mbalimbali katika maisha ,Ufanikiwe katika afya,ufanikiwe katika fedha ,ufanikiwe katika Roho ,umwabudu na umtumikiye na mwisho wa siku uweze kuishi naye milele katika uwepo wa Mungu.Njia za mafanikio zipo niyingi,zinafundishwa mashuleni ,vyuoni na hata sehemu za ibada.Ni wewe tut u mwenye utashi wa kuamua ama ufa maskini au uwe tajiri.(mzazi mwema ni Yule mwenye kuacha urithi hata kwa vitukuu) *NI HERI MIMBA ILIYOHARIBIKA KULIKO MTU ULIYEZALIWA UKAISHI HATA UFIKAPO KUWA MZEE NA MAZIKO YAKO YASIWE NA WATU.*Anzaa sasa kubadirika ili ufanikiwe.

RAYMOND  CHIMBUYA

## SOMO LA UJARIAMALI

Somo hili ni muhimu sana ,kwa sababu litakufanya ubadilike kutoka hapo ulipo na kuwa katika kiwango cha juu cha kiuchumu kama ukiamua kutoka ndani ya box nyeusi ul;ilofungiwa na adui shetani katika kupofusha akili na kukuamininisha kwamba fedha ni za shetani.

## HISTORIA YA FEDHA.

Ukisoma Biblia utaona fedha ni mali ya Bwana,Mbinguni kuna dhahabu safi,mimi Mungu nikupaye utajiri wa kupata fedha ili niweke Agano langu Imara.Vitu vyote vinaonyesha utajiri na fedha zilizoko Mbinguni ,pia inaonyesha wazi kwamba ukiwa na fedha inakuwa rahisi Mungu

kuweka Agano lake kwako,mtu maskini inakuwa ni vigumu sana kuweka Agano na Mungu kwa sababu ni rahisi kubadilika ,Kuna mifano mingi katika kipindi cha Mababa katika Biblia ambao walifanya Agano na Mungu wote walikuwa matajiri, mfano,IBRAHIMU,ISAAKA,YAKOBO.( Uf 21:21,5:1-2,5:6,11-12,Zab 24:1 ,Mwanzo 13:2-6,26:10-14)

## FAIDA ZA KUWA TAJIRI

1. Heshima- mithali 3:16-17

2. Ni Urithi wa Kristo:- 2kor 8:9

3. Agano la Mungu:-Isaya 45:3, Kumb 8:18, Torati 8:18, Kutoka 19:5 Torati 28:3

4. UTAWALA:-1Nyakati 29:12-28

5. THAWABU Mith 22:4

Kumbuka kwamba ukiwa na fedha unapata heshima, unakuwa na nguvu ya utawala,Biblia imeeleza tajiri atamtawala masikini na dhawabu.Hizi ni baadhi tu ya faida ya kuwa na fedha zipo nyingi ambazo utazipata wakati unaendelea kusoma kitabu hiki.

## NAMNA YA KUWA TAJIRI

1 Kubadili Mtazamo-Badili mtazamo kutoka katika mawazo hasi na kwenda katika mawazo chanya yenye kukupa mafanikinio

2 Kutunza kidogo ulichonacho/Kuweka akiba-Usitumiye zaidi ya kiapato chako, kumbuka kuweka akiba hata kama ni kidogo unachopata, kitakusaidia kuwa kingi(Haba na haba huajaza kibaba)

3 Kumtolea Mungu/anayesaidia masikini anamkopesha Mungu-Usiende nyumbani mwa Bwana pasipo kitu cha kumtolea Mungu, toeni kila mwanzo wa juma,kazi ya Mungu haiwezi kusonga mbele bila pesa,watumishi wa MUNGUwatakula kwa njia njia hiyo,ipowazi ki-Biblia.

4 Biashara-inakuingizia kipato,Biblia inasema afanyaye biashara ni kwa faida.Hakuna anyefanya biashara pasipo kuwa na faida, Mungu atakubariki katika biashara yako kwa kukupatia faida maana ni agano lake.Kumbuka asiyefanya kazi asile-kwa hiyo wanaofanyakazi ni kwa ajili ya chakula na siyo faida.Ukitaka kula tu,fanya kazi na ukitaka faida fanya biashara.

5 Kusaidia Yatima/Dini iliyo safi-unamkopesha Mungu-Saidia wenye shida, yatima, wajane na wenye hali ngumu ya maisha.

## Ujasiliamali ni nini?

Watu wengi wanadhana tofauti na neno Ujasiriamali,wengine wanasema ni kufanya biashara ,wengine wanadhana ya kuwa mtu ana ujasiri wa kuwa na mali,wengine wanasema ni kufanya biashara ndogondogo.Lakini mimi nasema,Ujasiriamali mpango maalumu kufanya kazi iliyo halali na kutenda kwa ustadi kwa kanuni na sheria zilizowekwa ili kuleta mafanikio ya Ki-Roho,kimwili kimaisha,ambao ni uwezo binafsi wa mtu wa kubadilisha mawazo hasi na kuwa katika mawazo chaya yenye vitendo yanayojumuisha ubunifu, kutengeneza kitu kipya na kuwa tayari kukabiliana katika hali yenye mtazamo chanya. Vilevile kuwa na uwezo wa kupanga na kuendeleza miradi ili kufikia malengo na  hii humsaidia mtu katika maisha yake ya kila siku akiwa nyumbani na katika jamii.

Ujasiriamali huwafanya waajiriwa kuwa na uelewa mpana kuhusu muktadha wa kazi zao na hatima ya maisha yao baada ya ajira kuwa katika nafasi nzuri katika kutumia fursa zilizopo. Pia ujasiriamali hutoa msingi kwa wajasiriamali kujenga shughuli za kijamii au kibiashara. Daktari wa Falsafa ndugu Olomi, (2009) anakubalina na dhana kuwa ujasiriamali kwa ujumla unaweza kuelezewa kama namna ya kufikiri, kutafakari na kutenda inayosababisha utengenezaji, uimarishaji, utambuzi na ufanyaji mpya wa vitu kwa maslahi ya mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu na jamii.

# KANUNI ZA UJASIRIAMALI ZA KI-MUNGU

**Uwe na uwezo wa kuona/maono/ndoto**

Uwe na uwezo wa kuona mwanya wa kibiashara na kuutafsiri huo mwanya wa kibiashara.

Katika kila tatizo ni fursa kwa Mjasiriamali, Mjasiriamali anapaswa kuwa na maono yenye tija ya kibiashara,

## Afya na Agano la Mungu

Afya ni jambo muhimu kwa mwanadamu ili uweze kutenda kazi, huwezi kufanyakazi kama huna afya njema. Unapaswa pia kufanya mazoezi mara kwa mara ili kuweka afya yako vizuri. Unapokuwa na afya njema na utajiri inakuwa rahisi Mungu kuweka agano na

wewe (kumb 8:17-18) *hapo usiseme moyoni mwako, nguvu zangu na uwezo wa mkono wangu ndio ulionipatia utajiri huo, bali utamkumbuka Bwana Mungu wako maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri, ili alifanye imara agano lake alilowapa baba zako kama hivi leo.*

## Uwe na lugha nzuri

Uwe na lugha mzuri inayoeleweka kwa wateja, lugha nzuri inavutia wateja, waswahili wanasema mali kauli. Unapokuwa na lugha mbofumbofu kwa wateja utawakimbiza mara utaanza kusema Ooh! Nahisi nimelogwa biashara haiendi kumbe unajiloga mwenyewe. *Maneno ya kinywa changu na mawazo ya moyo wangu yapate kibali mbele zako ee Bwana mwamba wangu na mwokozi wangu (zab 19:14).* Hivyo maneno yako yawe tofauti na wengine yenye hekima na busara. Nitakufundisha kwa habari ya ulimi, ulimi ni moto.Tumia vizuri ulimi wako

## TUMIA VIZURI ULIMI WAKO WEWE MTU WA MUNGU

. Kwa nini Biblia inafananisha moto na nguvu za ulimi?

MWANZONI mwa Oktoba 1871, moto mkubwa zaidi katika historia ya Marekani uliteketeza msitu ulio kaskazini mashariki mwa Wisconsin. Moto huo ulipozidi kuwaka, joto lake lilisababisha vifo vya watu zaidi ya 1,200 na kuteketeza miti bilioni mbili hivi. Huenda moto huo ulisababishwa na cheche kutoka kwenye treni zilizokuwa zikipita katika msitu huo. Tukio hilo linathibitisha ukweli wa maneno ya Yakobo 3:5: “Ni moto mdogo tu unaohitajika ili kuuwasha mwitu mkubwa!” Kwa nini Yakobo aliandika maneno hayo?

Tunapata somo la mfano huo katika mstari wa 6, unaosema hivi: “Ulimi ni moto.” Ulimi unawakilisha uwezo wetu wa kuzungumza. Kama moto, maneno yetu yana uwezo wa kusababisha madhara makubwa. Biblia inasema kwamba “kifo na uzima viko katika nguvu za ulimi.” (Met. 18:21) Bila shaka, hatuachi kuzungumza eti kwa sababu tunaogopa kusema jambo lenye kuumiza, kama vile ambavyo hatuachi kutumia moto eti kwa sababu unaweza kusababisha madhara. Jambo kuu ni kujizuia. Tukiutumia moto vizuri, unaweza kutusaidia kupika chakula, kupasha joto miili yetu, na kupata nuru wakati wa giza. Vivyo hivyo, tukidhibiti ulimi wetu, tutatumia nguvu zake kumheshimu Mungu na kuwanufaisha wengine.—Zab. 19:14.

### MAMBO MATATU YA UFAHAMU KATIKA KUSEMA

[3] Iwe tunazungumza kwa sauti au lugha ya alama, uwezo wa kuwasilisha mawazo na hisia zetu ni zawadi yenye kustaajabisha sana kutoka kwa Mungu. Tunaweza kutumiaje zawadi hiyo kujenga badala ya kubomoa? (Soma Yakobo 3:9, 10.) Tutazungumzia mambo matatu kuhusu usemi: wakati wa kusema, jambo la kusema, na jinsi ya kusema.

## Angalia wakati gani unapaswa kusema, na nani unataka kusema naye,na ni kwa nini unataka kusema

### Toa mifano ya wakati tunaopaswa "kukaa kimya."

4 Kuzungumza ni sehemu ya kawaida ya maisha yetu ya kila siku, hata hivyo hatuhitaji kuongea kila wakati. Biblia inasema kwamba kuna "wakati wa kukaa kimya." (Mhu. 3:7) Kukaa kimya wengine wanapozungumza kunaweza kuwa ishara ya heshima. (Ayu. 6:24) Kudhibiti ulimi wetu ili tusiseme mambo ya siri ya wengine kunaonyesha kwamba tuna busara na utambuzi. (Met. 20:19) Isitoshe, ni jambo la hekima kuzuia ulimi wetu tunapokasirishwa.—Zab. 4:4.

Tunaweza kuonyeshaje kwamba tunathamini uwezo wa kuzungumza tuliopewa na Mungu?

5 Kwa upande mwingine, Biblia inasema kwamba kuna "wakati wa kusema." (Mhu. 3:7) Ikiwa rafiki yako angekupa zawadi nzuri, bila shaka usingeificha zawadi hiyo. Badala yake, ungeonyesha kwamba unaithamini kwa kuitumia vizuri. Vivyo hivyo, tunapotumia uwezo wetu wa kuzungumza kwa hekima, tunaonyesha kwamba tunathamini zawadi hiyo kutoka kwa Yehova. Huenda hilo likahusisha kufunua hisia zetu, kueleza mahitaji yetu, kutiana moyo na kumsifu Mungu. (Zab. 51:15) Tunawezaje kujua 'wakati unaofaa zaidi wa kusema'?

6. Biblia inaonyeshaje umuhimu wa kuamua vizuri wakati unaofaa wa kusema?

6 Maneno ya Methali 25:11 yanaonyesha umuhimu wa kuamua wakati unaofaa wa kuzungumza. Andiko hilo linasema hivi: "Neno linalosemwa wakati unaofaa ni kama matunda ya mtofaa ya dhahabu kwenye chombo cha fedha kilichopambwa." Matofaa ya dhahabu yenyewe tu yangevutia. Kuyaweka kwenye chombo chenye rangi ya fedha, kungefanya yavutie zaidi. Vivyo hivyo, kuamua vizuri wakati unaofaa wa kuzungumza kunafanya maneno yetu yavutie na kuwasaidia wengine. Jinsi gani?

Ndugu zetu nchini Japani waliigaje mfano wa Yesu?

Tunataka kusema mambo ambayo msikilizaji wetu anahitaji hasa kuyasikia. Hata hivyo, tusipotambua wakati unaofaa wa kusema, maneno yetu yanaweza kueleweka vibaya. (Soma Methali 15:23.) Kwa mfano, mnamo Machi 2011 tsunami na tetemeko la ardhi liliharibu majiji mengi yaliyo mashariki mwa Japani. Zaidi ya watu 15,000 walipoteza maisha. Mashahidi wa Yehova pia waliathirika kama jirani zao, hata hivyo walijitahidi kutumia Biblia

kuwafariji watu waliokuwa wakiomboleza kila walipopata fursa. Lakini jirani zao wengi walikuwa Wabudha wenye imani kali, na hawakujua mengi au hawakujua kabisa mafundisho ya Biblia. Ndugu zetu walitambua kwamba muda mfupi tu baada ya tsunami kutokea haukuwa wakati unaofaa wa kuwaeleza jirani zao kuhusu tumaini la ufufuo. Badala yake, walitumia zawadi yao, yaani uwezo wa kuzungumza, kuwafariji na kuwaeleza ni kwa nini mambo mabaya kama hayo huwapa watu wazuri.

Yesu alijua wakati unaofaa wa kukaa kimya, na pia wakati unaofaa wa kusema. (Yoh. 18:33-37; 19:8-11) Wakati fulani aliwaambia hivi wanafunzi wake: "Bado nina mambo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili kwa sasa." (Yoh. 16:12) Mashahidi nchini Japani waliiga mfano wa Yesu. Miaka miwili na nusu baada ya tsunami, walishiriki katika kampeni iliyofanywa ulimwenguni pote ya kugawa trakti *Habari za Ufalme* Na. 38, yenye kichwa "Je, Kweli Wafu Wataishi Tena?" Wakati huo, watu wengi walikuwa tayari kukubali ujumbe wenye kufariji kuhusu tumaini la ufufuo, na wenye nyumba wengi walichukua nakala za trakti hiyo. Kwa kuwa utamaduni na imani za kidini hutofautiana kati ya mahali pamoja na pengine, tunahitaji kutumia utambuzi tunapoamua wakati unaofaa wa kusema.

Ni katika hali gani kuamua wakati unaofaa wa kuzungumza huleta matokeo mazuri?

[9] Kuna nyakati ambazo ni muhimu zaidi kutambua wakati wa kusema. Kwa mfano, huenda mtu akasema jambo linalotukasirisha. Litakuwa jambo la busara kutafakari kwanza ikiwa jambo hilo ni zito hivi kwamba tunahitaji kusema kitu. Ikiwa tunahitaji kusema, basi halingekuwa jambo la hekima kuongea na mtu aliyetukosea tukiwa tumekasirika, kwa kuwa tunaweza kuongea bila kufikiri. (Soma Methali 15:28.) Isitoshe, tunahitaji kutambua wakati unaofaa wa kuzungumza kuhusu kweli na watu wetu wa ukoo ambao si Mashahidi. Tunataka wamjue Yehova, hata hivyo ni lazima tuwe wenye subira na utambuzi. Kusema maneno yanayofaa kwa wakati unaofaa kunaweza kuwafanya wawe tayari kusikiliza.

## JAMBO LA KUSEMA

(a) Kwa nini tunapaswa kuchagua kwa uangalifu maneno tunayosema? (b) Toa mfano wa maneno yenye kuumiza.

[10] Maneno yana nguvu za kuumiza na kuponya. (Soma Methali 12:18.) Kutumia maneno yanayoumiza ni jambo la kawaida katika ulimwengu wa Shetani. Leo, burudani nyingi huwachochea watu 'kunoa ulimi wao kama upanga' na kufyatua 'maneno machungu kama mishale.' (Zab. 64:3) Mkristo anapaswa kuepuka mazoea hayo hatari. Mfano mmoja wa "maneno machungu" ni kejeli, yaani maneno yaliyokusudiwa kuwadhalilisha au kuwashutumu wengine. Mara nyingi kejeli huanza kama ucheshi, lakini inaweza kugeuka haraka na kuwa maneno yasiyo ya heshima au matusi. Kejeli zenye kuumiza ni mojawapo ya matukano ambayo Wakristo wanapaswa 'kuyaondolea mbali.' Ucheshi unaweza kufanya mazungumzo yawe yenye kufurahisha. Hata hivyo, tunahitaji kuepuka mtego wa kuwachekesha watu kwa kutumia maneno yasiyofaa au kebehi ambazo zitawaumiza au kuwadhalilisha wengine. Biblia inatuhimiza hivi: "Neno lililooza na lisitoke kinywani mwenu, bali neno lolote ambalo ni jema kwa ajili ya kujenga kulingana na uhitaji, ili liwape wasikiaji lile linalofaa."—Efe. 4:29, 31.

11. Kuna uhusiano gani kati ya moyo wetu na kuchagua maneno yanayofaa?

[11] Yesu alifundisha kwamba "kinywa kinasema kutokana na mambo yaliyojaa katika moyo." (Mt. 12:34) Hivyo, kuchagua maneno yanayofaa huanzia moyoni. Kwa kawaida, maneno yetu hufunua hisia zetu kuelekea watu wengine. Ikiwa kweli tunawapenda na kuwajali watu, yaelekea tutazungumza mambo yanayofaa na yanayowajenga wengine.

12. Tunaweza kuboreshaje uwezo wetu wa kuchagua maneno yanayofaa?

[12] Jitihada na busara inahitajika ili tuchague maneno yanayofaa. Hata Mfalme Sulemani mwenye hekima "alitafakari na kutafuta kwa bidii" ili apate "maneno yenye kupendeza na kuandika maneno sahihi ya kweli." (Mhu. 12:9, 10) Je, ni vigumu kwako kupata "maneno yenye kupendeza"? Ikiwa ndivyo, basi huenda unahitaji kujifunza maneno mapya. Njia moja ya kufanya hivyo ni kuchunguza jinsi maneno yanavyotumiwa katika Biblia na machapisho yetu ya Kikristo. Jifunze maana ya maneno usiyoyajua. Zaidi ya yote, jifunze kutumia maneno kwa njia itakayowasaidia wengine. Tunasoma hivi kuhusu uhusiano uliopo kati ya Yehova na Mwana

wake mzaliwa wa kwanza: “Yehova amenipa ulimi wa waliofundishwa, ili nijue jinsi ya kumjibu neno yeye aliyechoka.” (Isa. 50:4) Kutafakari kabla ya kusema kunaweza kutusaidia kupata maneno yanayofaa. (Yak. 1:19) Tunaweza kujiuliza hivi, ‘Je, kweli maneno haya yatawasilisha kile ninachotaka kusema? Maneno yangu yatakuwa na matokeo gani kwa mtu anayenisikiliza?’

13. Kwa nini ni muhimu kutumia maneno yanayoeleweka kwa urahisi?

[13] Katika Israeli, tarumbeta zilitumika kuwakusanya watu, kuwatawanya, au kuwachochea wanajeshi waanze mapambano. Hivyo, Biblia inafananisha mlio wa tarumbeta na uhitaji wa kutumia maneno yanayoeleweka kwa urahisi. Ikiwa tarumbeta ingetoa mlio usiojulikana, hilo lingeweza kusababisha maafa makubwa kwa wanajeshi vitani. Vivyo hivyo, ikiwa maneno yetu hayako wazi au hayaeleweki, yanaweza kuwachanganya au kuwapotosha wengine. Hata hivyo, tunapojitahidi kutumia maneno yaliyo wazi na yanayoeleweka kwa urahisi, inafaa pia tuzungumze kwa adabu na busara.—Soma 1 Wakorintho 14:8, 9.

14. Toa mfano unaoonyesha kwamba Yesu alitumia maneno rahisi na yanayoeleweka.

[14] Yesu aliweka mfano bora zaidi wa kuchagua maneno yanayofaa. Fikiria hotuba yake fupi iliyoandikwa kwenye Mathayo sura ya 5 hadi ya 7. Yesu hakutumia maneno yenye utata au madoido; wala hakutumia lugha kali au maneno yenye kuumiza. Badala yake, alichagua maneno yaliyo wazi na rahisi ambayo yaligusa mioyo ya wasikilizaji wake. Kwa mfano, Yesu alitaka watu wasiwe na mahangaiko kuhusu uhitaji wao wa kila siku wa kupata chakula, hivyo akawaeleza jinsi ambavyo Yehova huwalisha ndege wa mbinguni. Kisha, akiwalinganisha wasikilizaji wake na ndege, aliwauliza hivi: “Je, ninyi si bora kuliko wao?” (Mt. 6:26) Naam, maneno hayo rahisi na yanayoeleweka yaliwatia moyo sana! Acheni sasa tuzungumzie jambo la tatu muhimu kuhusu usemi.

## JINSI YA KUSEMA

Kwa nini tunapaswa kuzungumza kwa fadhili?

[15] Ni muhimu sana pia kuzingatia jinsi tunavyosema jambo fulani. Yesu alipozungumza katika sinagogi lililokuwa kwenye mji wake wa nyumbani, Nazareti, watu 'walistaajabia maneno yenye kuvutia sana yaliyokuwa yakitoka kinywani mwake.' (Luka 4:22) Maneno yenye kuvutia hugusa moyo na kamwe hayadhoofishi nguvu za ulimi wetu. Kwa kweli, maneno yenye kuvutia au yenye fadhili yanaweza kuwashawishi watu wakubali mambo tunayosema. (Met. 25:15) Tunaweza kuiga maneno yenye kuvutia ya Yesu kwa kuwa wenye adabu na kujali hisia za wengine. Kwa mfano, alipoona jitihada ambazo watu walifanya ili wamsikilize, Yesu alichochewa na huruma naye "akaanza kuwafundisha mambo mengi." (Marko 6:34) Hata alipotukanwa, Yesu hakujibu kwa maneno makali.(1 Pet. 2:23)
(a) Tunawezaje kumwiga Yesu tunapozungumza na washiriki wa familia au rafiki zetu wa karibu kutanikoni? (Tazama picha mwanzoni mwa makala hii.) (b) Toa mfano unaoonyesha faida za kuzungumza kwa fadhili.

Huenda ikawa vigumu kuzungumza kwa upole na kwa busara tunapoongea na mtu tunayemjua vizuri. Labda mtu huyo ni mshiriki wa familia au rafiki yetu wa karibu kutanikoni. Huenda

tukahisi kwamba hatuhitaji  kuwa waangalifu tunapozungumza. Je, Yesu alihisi kwamba uhusiano wake wa karibu na wanafunzi wake ulimpa uhuru wa kuzungumza nao kwa ukali? La hasha! Wafuasi wake wa karibu walipoendelea kubishana kuhusu ni nani aliye mkubwa kati yao, Yesu aliwarekebisha kwa maneno ya upole na akawapa mfano wa mtoto mdogo. (Marko 9:33,37) Wazee humwiga Yesu wanapotoa ushauri kwa "Roho ya upole.("Gal. 6:1)

[17] Hata ikiwa mtu amesema jambo linalotukasirisha, kujibu kwa upole kunaweza kuwa na matokeo mazuri. (Met. 15:1) Kwa mfano, kijana wa mama mmoja asiye na mwenzi, alikuwa

akifanya mambo mabaya ilhali akidai kumtumikia Yehova. Dada fulani Mkristo mwenye nia nzuri alimwambia hivi mama ya kijana huyo: “Inasikitisha sana kwamba umeshindwa kumzoeza mtoto wako.” Mama huyo alitafakari kidogo na kujibu hivi: “Ni kweli kwamba mambo hayaendi vizuri sasa, hata hivyo mazoezi yake ni kazi endelevu. Zungumza nami baada ya Har–Magedoni; kisha tutajua mambo yalivyo.” Jibu hilo la upole lilisaidia kudumisha amani kati ya akina dada hao, na lilimtia moyo kijana huyo, ambaye alisikia mazungumzo hayo. Alitambua kwamba mama yake hakuwa amekata tamaa. Jambo hilo lilimchochea aache kushirikiana na marafiki wabaya. Baadaye alibatizwa, na kutumikia Betheli. Iwe tupo na ndugu zetu, familia yetu, sikuzote maneno yetu yanapaswa kuwa ‘yenye neema na yenye kukolezwa chumvi(.Kol. 4:6).
Kuiga mfano wa Yesu kunaweza kutusaidiaje tutumie vizuri nguvu za ulimi wetu?
Kwa kweli, uwezo wetu wa kufunua hisia na mawazo yetu kwa maneno unastaajabisha sana! Acheni basi tuige mfano wa Yesu kwa kuamua wakati unaofaa wa kusema, kujitahidi kuchagua maneno yanayofaa, na kuzungumza kwa fadhili. Tukifanya hivyo, nguvu za ulimi wetu zitawaponya wale wanaotusikiliza na kumfurahisha Yehova, ambaye ndiye Mpaji wa zawadi hiyo yenye thamani, yaani uwezo wa kuzungumza.

## Uwe na moyo wa kufanya kazi

Usiwe mvivukatikashughuli zako, fanya kazi kwa moyo. Unapokuwa mvivu unahatarisha biashara yako kisha itakufa kabisa. Anaependa kulala atakufa maskini. Biblia ina mpango mkubwa wa kusema kuhusu uvivu. Mithali imejawa na hekima kuhusu uvivu na onyo kwa mtu mvivu. Mithali inatuambia kwamba mtu mvivu anachukia kazi: "Matakwa yake mtu mvivu humfisha, kwa maana mikono yake hukataa kufanya kazi." (Mithali 21:25)

Mtu awaye yote apendaye kulala mtu huyo ni mvivu: "Kama vile mlango ugeukavyo katika bawaba zake,kadhalika mtu mvivu katika kitanda chake" ( Mithal 26:14); yeye anatoa visingizio: "Mtu mvivu husema, simba yuko njiani , simba yuko katika njia kuu'" (

Mithali 26:13); anapoteza muda na nishati: "Yeye naye aliye mvivu katika kazi yake, Ni ndugu yake aliye mharabu" (Mithali 18: 9 ); yeye anaamini kuwa ana busara, lakini ni mjinga: "Mtu mvivu ni mwenye hekima machoni pake, Kuliko watu saba wawezao kutoa sababu"(Mithali26:16)

Mithali pia inatuambia mwisho uliohifadhiwa kwa ajili ya wavivu: mtu mvivu anakuwa mtumishi (au mdaiwa): "Mkono wa mwenye bidii utatawala; bali mvivu atalipishwa kodi." (Mithali 12:24); mustakabali wake ni wa giza: "Mtu mvivu hataki kulima wakati wa baridi; hivyo wakati wa mavuno ataomba,hana kitu "(Mithali 20: 4); anaweze kuja kuwa maskini: "Nafsi ya mtu mvivu hutamani asipate kitu;bali nafsi ya mwenye bidii itanenepeshwa.

Hakuna nafasi kwa uvivu katika maisha ya Mkristo. Muumini mpya anafundishwa hivyo kwa kweli "... kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2: 8 -9). Lakini muumini anaweza kuwa mzembe kama yeye anaamini kimakosa Mungu hatarajii matunda kutoka kwa maisha yaliyobadilishwa. "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo" (Waefeso 2:10). Lakini mtu atasema, wewe unayo imani, nami ninayo matendo. Nionyeshe imani yako pasipo matendo, nami nitakuonyesha imani yangu kwa njia ya matendo yangu; Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo na matendo imekufa.(Yakobo 2:18, 26). Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya. (2 Wakorintho 5:17).

Katika asili yetu mpya, tumetiwa hali mpya kwa bidii na uzaaji kutoka kwa upendo kwa Mwokozi wetu ambaye alitukomboa. Mwelekeo wetu wa kale kwa uvivu na dhambi

zingine zote,tamaa ya kutaka kuishi maisha ya kumcha Mungu imekuwa badala yake: "Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji" (Waefeso 4:28). *Nakuombea Neema ya Bwana wetu Yesu kristo ikufunguwe macho, Kwa JINA LA YESU KRISTO.*

## Muda.(TIME MANAGEMENT)

Muda ni muhimu sana, watu wengi wanapoteza muda wao kuzungumzia mambo yasiofaa, muda ni mali,usipoteze muda kwa kuzungumza umbea,mizaa au blablaaa,Jitahidi muda mwingi uzungumziye mambo ya Mungu na biashara mbalimbali kwa waliofanikiwa.”Na wana Isakari,watu wenye akili za kujua nyakati,kuyajua yawapasayo waisrael,wayatende vichwa vyao walikuwa watu mia mbili na ndugu zao wote walikuwa chini ya amri zao.( Mambo ya Nyakati 12;32,3:1) Hapa tunajifunza namna walivyotumia wakati vizuri.Kwa kila jambo kuna majira yake,na wakati wa kusudi chini ya Mbingu.Unajifunza  jinsi gani kila wakati unatakiwa kuutendea haki,usipoteze wakati,kuna wakati wa kulala, lala,wa mazoezi fanya mazoezi,wa kufanya biashara fanya biashara,na wakati wa kuomba omba kwa bidii.

## Mtandao

Mtandao ni jambo muhimu katika biashara ili kuongeza wateja.Katika mtandao wako chagua aina ya marafiki.Usikubali kuwa na marafiki wenye mawazo mgando.Una uhuru wa kuchagua marafiki,huwezi kuchagua mama,lakini baba mama anaweza akakuchagulia. Pia wewe unaweza kuchagua marafiki, ukigundua rafiki yako hamwezi

kwenda pamoja katika maono yako ya mafanikio ,yeye kazi yake ni kukukatisha tamaa achana naye.Marafiki wazuri kwako ni wale ambao mtaendana na maono yako,unaweza



kuchagua marafiki wenye faida kwako kama vile wataalamu mbalimbali *mfano wanaweza kuwa Wanasheria,Madaktari au Watumishi wa Mungu wenye ustadi wa kumjua Mungu katika kanuni zake.* Leo, kupitia teknolojia tunaweza kupata mamia, au hata maelfu ya "marafiki" kwenye mitandao ya kijamii kama vile facebook, twiter,istagram,skype,whatsaap na nyingine nyingi zinazoibuka kila kukicha, kwa kuongeza tu majina yao kwenye orodha yetu ya anwani katika kompyuta. Pia, tukitaka kukatisha "urafiki" na yeyote kati yao, tunafuta tu jina lake (block) kutoka kwenye orodha yetu. Bila shaka, kama watu wengi unakubali kwamba ni muhimu kuwa na marafiki wa kweli. Huenda pia umetambua kwamba urafiki unahusisha mengi kuliko kuongeza majina kwenye orodha ya kompyuta au simu yako. Rafiki wa kweli anapaswa kuwa na sifa unazopenda wewe(ndege wa rangi moja huruka pamoja). Biblia inatuhimiza tuwe na marafiki wa aina mbalimbali. Kukubali maoni ya wengine na kutobagua watu kunaweza kuboresha maisha yako, na pia kufanya watu wapendezwe nawe. (2 Wakorintho 6:13)

## Unawezaje kupata marafiki mzuri? Ni mambo gani yanayohitajika ili kupata marafiki wa kudumu?

### Kujali watu

**Urafiki WA kweli unahusisha vitendo Na siyo Kwa maneno tu, rafiki mzuri anajua majukumu yake, na ni mwenye kujali. Ni vizuri uwe na urafiki unahusisha pande mbili, na kila mmoja anapaswa kutimiza sehemu ya mahitaji yake.(win win situation). Pia kuna faida za kufanya hivyo. Jiulize, 'Je, upo tayari kujitoa kutumia muda na mali zako kwa ajili ya rafiki yako?' Kumbuka, ili upate rafiki mzuri, *wewe* mwenyewe unapaswa kuwa rafiki mzuri.**

**Swali: "Je, Mkristo anapaswa kufanya biashara na asiyeamini?"**

**Jibu:** Swali ikiwa Mkristo anapaswa kungia katika biashara na asiyeamini ni moja wapo la kawaida. Kitabu mara nyingi-hunukuliwa ni "Msifungiwe nira pamoja n wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa, kwa maana pan urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza?" (2 Wakorintho 6:14). Mara nyingi, mstari huu huchukuliwa kuwa katazo kwa Wakristo dhidi ya kuoa wasio Wakristo. Ndoa pasi itakuwa dhahiri hapa, lakini kuna kitu katika mazingira ambapo hukiweka kuwa cha ndoa. Kila aina zote za "kutiwa nira pamoja" zimekataliwa-ndoa, urafiki wa karibu, na, katika matukio mengi, ushirikiano wa biashara.

Amri hii ina maana kwamba kuna tofauti kubwa kati ya muumini na kafiri. Kwa ujumla, motisha, malengo, na mbinu za Kikristo ni kinyume na zile za mtu wasiyeamini. Imani hubadilishaa tabia ya mtu. Tamaa ya Mkristo kuu katika maisha ni kumtukuza Bwana Yesu na kumpendeza Yeye katika mambo yote; kafiri si bora, tofauti na malengo hayo. Kama mbinu ya Mkristo na malengo katika biashara ni sawa na mbinu na malengo ya

kafiri, Mkristo vile vile anapaswa kutathmini pakubwa sana mahitaji yake tena nakufikiria upya vipaumbele vyake.

RAYMOND  CHIMBUYA

Pili Wakorintho 6:14 unaendelea kuuliza, "Je, kuna ushirika gani kati ya nuru na giza?" Watu wanasemekana kuwa "katika ushirika" wakati wao hushiriki kitu. Washirika wa biashara ni umoja katika njia hiyo wao lazima kushiriki mambo-kile ambacho ni cha mmoja pia ni mali ya mwingine. Hiki hasa ndio maana ya "ushirika." Pamoja na kanuni hizi katika akili, ni bora ili kuepuka kuunganishwa pamoja na wasioamini katika biashara. Kama Mkristo kweli hutafuta kuheshimu Bwana kwa njia ya biashara, migogoro na wasioamini biasharani haiwezi. "Je, watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?" (Amosi 3: 3).

**Anza na wewe**

Ndiposa unahitaji kujitahidi ili kusitawisha urafiki. Anza Kwa kuwa rafiki mzuri wewe mwenyewe. Jitahidi sana kuonyesha upendo na kupendezwa na wengine. Na uwe tayari kutumia muda wako inapohitajika." *"Kama vile mnavyotaka watu wawatendee ninyi, watendeeni wao vivyo hivyo. Muwe na mazoea ya kuwapa watu, na watu watawapa ninyi."* (Luka 6:31, 38)

Ndiposa "Watu wengi leo wana ubinafsi badala ya ukarimu. Basi, inapendeza sana mtu anapokuonyesha upendo bila kutazamia kwamba utamlipa chochote huyo ni rafiki mwema.

*"Kila mtu lazima awe mwepesi kuhusu kusikia, si mwepesi wa kusema, si mwepesi wa ghadhabu."* Marafiki wa kweli hupenda kusikilizwa. (Yakobo 1:19)

Hata hivyo, kutawala mazungumzo kunaonyesha kwamba tunafikiri maoni yetu ni bora kuliko ya wengine. Kwa hiyo, sikiliza kwa makini rafiki anapokueleza maoni yake ya moyoni na

mahangaiko yake. Pia, usikasirike akikuambia ukweli. “Vidonda vinavyosababishwa na mpenzi ni vya uaminifu.” ( Methali 27:6)

RAYMOND  CHIMBUYA

## Msitengane wakati wa mafanikio

Jinsi unavyozidi kuwa karibu na rafiki yeko ndivyo inavyokuwa rahisi kutambua makosa yake. Kama sisi, rafiki zetu si wakamilifu. Kwa hiyo, hatupaswi kutarajia ukamilifu kutoka kwa rafiki zetu. Badala yake, ni vizuri kupendezwa na sifa zao nzuri na kutokazia fikira makosa yao.Urafiki wa kweli hauwezi kusitawi bila mawasiliano ya kawaida. Kwa hiyo, zungumzieni mambo yanayowapendeza. Msikilize rafiki yako, na uheshimu maoni yake. Ikiwezekana, mpongeze na umtie moyo. Nyakati nyingine, huenda rafiki akahitaji ushauri au hata kurekebishwa, na huenda isiwe rahisi kufanya hivyo. Hata hivyo, rafiki mshikamanifu anajua jinsi ya kumkosoa mwenzake na kutoa ushauri kwa busara.*“Sisi sote hujikwaa mara nyingi. Ikiwa yeyote hajikwai katika neno, huyo ni mtu mkamilifu, anayeweza kuuongoza kwa lijamu mwili wake wote pia.”* (Yakobo 3:2)

Kutambua ukweli huo kutatusaidia kuwaelewa rafiki zetu. Hilo litafanya tupuuze kasoro ndogo na mambo yanayoweza kutuudhi. Biblia inasema hivi: *“Endeleeni kuvumiliana na kusameheana kwa hiari ikiwa yeyote ana sababu ya kulalamika juu ya mwingine Lakini, zaidi ya mambo haya yote, jivikeni upendo, kwa maana huo ni kifungo kikamilifu cha muungano.(*Wakolosai 3:13, 14)

## Njia Mbalimbali za Kupata Mafanikio

Mwanadamu anafanikiwa katika hatua zote kwa kupata njia bora kabisa ya maisha ambayo inatokana na kufuata viwango vya Mungu na kuishi kutokana na kusudi la Mungu kwa wanadamu. Biblia inasema kwamba mtu anayeishi maisha ya mafanikio kama ilivyo kusudi la Mungu “atakuwa kama mti uliopandwa kando ya vijito vya maji, ambao hutoa matunda yake

katika majira yake na ambao majani yake hayanyauki, na *kila jambo analofanya litafanikiwa."*(Zaburi 1:3.)

RAYMOND CHIMBUYA

Hata kama sisi ni wakosaji, tunaweza kufanikiwa maishani! Je, hilo linakuvutia? Yumkini yakupsa kufuata kanuni za Biblia ambazo zinaweza kukusaidia ufikie lengo la mafanikio na kukuthibitishia waziwazi kwamba kwa kweli mafundisho ya Biblia ni hekima inayotoka kwa Mungu.(Yakobo 3:17)

## Uwe na Mawazo Yanayofaa Kuhusu Pesa

*"Kupenda pesa ni chanzo cha mambo mabaya ya namna zote, na kwa kujitahidi kufikia upendo huo wengine wamejichoma wenyewe kila mahali kwa maumivu mengi."* (1 Timotheo 6:10) Kuwa na pesa nyingi siyo tatizo,tatizo ni kwa jinsi gani umepata hizo pesa na unazitumiaje hizo pesa. Kwa kuwa sisi sote tunahitaji pesa ili Kuishi kwa furaha na kupata heshima pamoja na kutunza vizuri familia zetu. Mtu kamwe hawezi kwenda Mbinguni kwa sababu ya umaskini wake,la hasha,Mtu atamwona Mungu kwa kuwa na matendo yanayompendeza Mungu na wala mtu hawezi kwenda mbinguni kwa utajiri wake bali ni kwa kujali watu na kuwasaidia wajane(Yakobo 1:27)

## Imarisha Roho ya Ukarimu

"Kuna furaha zaidi katika kutoa kuliko ilivyo katika kupokea hata hivyo usitowe kupita kiasi ,ingawa kuwapa watu vitu au kumsaidia mtu mara kwa mara kunaweza kumfanya mtu awe na furaha ya muda, roho ya ukarimu inaweza kumfanya awe na furaha *ya kudumu.* Ni kweli kwamba kuna njia mbalimbali za kuonyesha ukarimu. Mojawapo ya njia bora na inayothaminiwa sana ni kutenga wakati ili kuwa pamoja na watu na kufanya mambo nao. (Matendo 20:35)

## Samehe kwa Hiari

Basi msamehe jirani yako kama unavyopenda kusamehewa na Mungu“Endeleeni . . . kusameheana kwa hiari ikiwa yeyote ana sababu ya kulalamika juu ya mwingine. Kama vile MUNGU alivyowasamehe ninyi kwa hiari, nanyi fanyeni vivyo hivyo pia.*”* (Wakolosai 3:13)

Kizazi hiki watu wengi hawako tayari kusamehe,ni kiazi za ukaidi,ni kizazi cha kisasi badala ya kuonyesha rehema. Matokeo ni nini? Wanapotukanwa wanatukana, nao hulipiza jeuri kwa jeuri kama nyakati za Musa za jino kwa jino.

Unawezaje kusamehe zaidi? Anza kwa kujichunguza kwa unyoofu. Je, nyakati nyingine huwakasirishi watu? Unafurahi wanapokusamehe? Kwa hiyo, mbona usiwaonyeshe wengine rehema? (Mathayo 18:21-35)

Pia ni muhimu kujizuia. “Hesabu moja hadi kumi” au tafuta wakati ili utulize hasira. Tambua kwamba kujizuia si udhaifu. “Asiye mwepesi wa hasira ni bora kuliko mwanamume mwenye nguvu,” ( Methali 16:32).

## Ishi Kulingana na Viwango vya Mungu

*“Amri ya Mungu ni safi, huyafanya macho yang’ae.”* (Zaburi 19:8) Kwa ufupi, viwango vya Mungu vinatufaidi, kimwili, kiakili, na kihisia. Vinatulinda dhidi ya mazoea yenye kudhuru kama vile, kutumia dawa za kulevya, kulewa, ukosefu wa maadili, na kutazama ponografia (picha au habari za ngono). (2 Wakorintho 7:1; Wakolosai 3:5)

Huenda mazoea hayo yakatokeza madhara mabaya kama vile uhalifu, umaskini, kutoaminiana, kuvunjika kwa familia, matatizo ya kiakili na kihisia, magonjwa, na kifo cha mapema.

Kwa upande mwingine, wale wanaoishi kulingana na viwango vya Mungu wanakuwa na mahusiano mazuri, pia wanajiheshimu, na kuwa na amani ya akili.(Isaya 48:17, 18)

RAYMOND  CHIMBUYA

Mungu anasema wazi ya kwamba YEYE NDIYE “anayekufundisha ili ujifaidi mwenyewe, Yeye anayekufanya uende katika njia unayopaswa kutembea ndani yake.” Kisha anaongeza hivi: “Laiti ungesikiliza amri zangu! Ndipo amani yako ingekuwa kama mto, na uadilifu wako kama mawimbi ya bahari.” Ndiyo, Muumba wetu anatutakia maisha bora zaidi. Anataka ‘tuende katika njia’ ya mafanikio ya kweli.

## Onyesha Upendo Usio na Ubinafsi katika maisha

Mara zote onyesha upendo usio na kikomo *“Upendo hujenga.”* (1 Wakorintho 8:1) Je, unaweza kuwazia maisha yasiyo na upendo? Yangekuwa maisha yasiyo na maana kama nini! “Ikiwa sina upendo [kwa wengine], mimi si kitu.Sipati faida hata kidogo,” akaandika Paulo, mtume Mkristo aliyeongozwa na roho ya Mungu (1 Wakorintho 13:2, 3.)

Upendo unaotajwa hapa si ule wa kimahaba au wa kibaby hapana ,huwo wa kibaby una mahali pake panapofaa. Badala yake ni upendo unaodumu ambao unaongozwa na kanuni za Mungu.* (Mathayo 22:37-39) Isitoshe, mtu haonyeshwi tu upendo huo bali anauonyesha kwa matendo. Upendo wa Kristo ambao hujenga. Pia, unatusaidia tuwe na uhusiano mzuri na wengine hasa washiriki wa familia.(1 Wakorintho 13:4-8.)

## Tambua Uhitaji Wako wa Kiroho mara zote

“Wenye furaha ni wale wanaotambua uhitaji wao wa kiroho.” (Mathayo 5:3) Tofauti na wanyama, wanadamu wana uwezo wa kuthamini mambo ya kiroho. Kwa sababu hiyo, sisi

hujiuliza maswali kama haya, Ni nini kusudi la uhai? Je, kuna Muumba? Ni nini hutupata tunapokufa? Wakati ujao utakuwaje?

Ulimwenguni pote, mamilioni ya watu wanyoofu wametambua kwamba Biblia inajibu maswali hayo. Kwa mfano, swali la mwisho linahusiana na kusudi la Mungu kwa wanadamu. Kusudi hilo



ni nini? Ni kwamba dunia iwe paradiso inayokaliwa na watu wanaompenda Mungu na viwango vyake. “Waadilifu wenyewe wataimiliki dunia, nao watakaa milele juu yake.”( Zaburi 37:29)

Ni wazi kwamba Muumba wetu anataka tufanikiwe kwa muda mrefu zaidi kuliko miaka 70 au 80 tu. Anataka tufanikiwe milele! Kwa hiyo, sasa ndio wakati wako wa kujifunza kuhusu

Muumba wako. Yesu alisema: “Uzima wa milele ndio huu, waendelee kupata ujuzi juu yako wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na juu ya yule uliyemtuma, Yesu Kristo.” (Yohana 17:3)

## MAMBO YATAKAYOKUFANYA UPATE MAFANIKIO ZAIDI HAPA DUNIANI NA MBINGUNI

▪ Hofu ya Mungu. “Kumwogopa Yehova ndio mwanzo wa hekima.”(Methali 9:10.)
The faer of God is the wisdom.

▪ Chagua marafiki kwa hekima. “Anayetembea na watu wenye hekima atakuwa na hekima, lakini anayeshirikiana na wajinga atapatwa na mabaya.”(Methali 13:20.)
Ndege wa rangi moja huruka pamoja.

▪ Epuka Ulevi kula kupita kiasi. “Mlevi na mlafi watakuwa maskini.”(Methali 23:21)

▪ Usilipize kisasi kisasi ni cha Bwana “Msimlipe yeyote uovu kwa uovu.”(Waroma 12:17)
Acha Mungu aseme na maadui zako,kisasi ni cha Bwana.

▪ Fanya kazi kwa bidii. “Ikiwa yeyote hataki kufanya kazi,  na asile chakula.(2 Wathesalonike 3:10)
Ni Mungu pekee amekupa nguvu ya kufanya kazi,ondoa ulegevu ,tia bidii katika kazi.

▪ Fuata ile Kanuni Bora iliyo ya Bwana. “Mambo yote mnayotaka watu wawatendee ninyi, lazima mwatendee wao pia vivyo hivyo.”(Mathayo 7:12)
Mungu ni upendo ,ukiwa na upendo Mungu yupo ndani yako,tuishi katika kanuni za Mungu na siyo mbinu zako.

▪ Chunga sana ulimi wako. “Yeye ambaye anapenda uzima na kuona siku zilizo njema, na auzuie ulimi wake kutokana na yaliyo mabaya.”(1 Petro 3:10)

RAYMOND  CHIMBUYA

**Akiba.**

Usitumiye fedha kiasi kinachozidi kipato chako, jifunze kuweka akiba

"Bibilia inasema nini kuhusu utumiaji mzuri wa pesa zako?"

Jibu: Bibilia imesema mengi kuhusu usimamizi wa pesa. Kuhusu kukopa, Bibilia kwa jumla inasema hivi:Angalia Methali 6: 1-5; 20:16; 22: 7, 26-27 (“Tajiri humtawala maskini, Naye akopaye ni mtumwa wake akopeshaye.Usiwe mmoja wao wawekao rahani; Au walio wadhamini kwa deni za watu; Kama huna kitu cha kulipa; Kwani ukaondolee kitanda chao chini yako”). Bibilia inatuonya kujiwekea utajiri na inatuambia kutafuta utajiri wa ki-Roho MMBADAL WAKE. Methali 28:20, “Mtu mwaminifu atakuwa na baraka tele; Lakini afanye haraka kuwa tajiri hakosi ataadhibiwa.” Angalia pia Methali 10:15; 11:4; 18:11; 23:5.

Hapa tunajifunza Kwa habari ya utajiri wenye Baraka na siyo uletao machafuko.

Methali 6:6-11 inasema hivi, maarifa kuhusu uzembe na utumiaji mpya wa fedha ambao utatokea. Tumeambiwa tuwatizame mchwa vile walivyo na bidii ambayo wafanya kazi kuweka akiba chakula. Ufahamu huo pia watuonya kulala wakati tunastahili kufanya kazi kwa kitu ambacho ni cha faida. “Mtu goigoi” ni mvivu, mtu mzembe ambaye atapumzika badala ya kufanya kazi. Hatima yake imeakikishwa – umaskini na hitaji. Kwa upande mwingine mwisho wake ni mtu aliyejawa na nia ya kujiwekea utajiri. Mtu kama huyo kulingana na Mhubiri 5:10 hatajwi kuwa na utajiri wa kutosha wa kumridhitisha na ataendelea kunyakua zaidi na zaidi. Apendaye fedha hatashiba fedha,wala apendaye wingi,hatashiba maongeo,haya pia ni ubatili.Timotheo wa Kwanza 6:6-11 pia yatuonya kuhusu mitego ya kutamani utajiri.

***NB;hapa tunajifunza wazi kwamba ,fedha isikufanye umwache Mungu,yatupasa kuwa fedha na kuridhika,katazokuuu ni kutoridhika na ulichonacho.Kwa hiyo ukiwa na fedha usifarakane na imani.***

Badala ya kuthamani kujiwekea utajiri, mfano wa Bibilia ni ule wa kutoa, sio kupokea. “Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu” (2 Wakorintho 9:6-7). Pia tumetiwa moyo tuwe watunzaji wema wa kile ambacho Mungu ametupa. Katika Luka 16:1-13 yesu alipeana mfano wa mtu mtunzaji asiye mwaminifu na kutuonya juu ya utunzaji mpaya. Maadili ya hadhiti ni “Basi kama ninyi hamkuwa waaminifu katika mali ya udhalimu, ni nani atakayewapa iliyo yenu wenyewe?”(aya ya 11). Pia tumewajibika kuwatafutia risiki wale wa



nyumba yetu, vile 1 Timotheo 5:8 yatukumbusha: “Lakini mtu ye yote asiyewatunza walio wake, yaani wale wa nyumbani mwake hasa, ameikana Imani, tena ni mbaya kuliko mtu asiyeamini.”

Kwa ufupi, nini Bibilia yasema kuhusu utunzaji bora wa fedha? Jibu linaweza wekwa kwa mukhtasari kwa neno moja-maarifa. Tunastahili kuwa wa maarifa na fedha zetu. Tunastahili kuweka akiba fedha, bali si kuzivuja. Tunastahili kutumia fedha, lakini kwa mwelekeo na

kadirio. Tunastahili kumpatia Mungu, kwa ukarimu na thabihu. Tunastahili kutumia fedha kuwazaidia wengine, lakini kwa utambuzi na uongozi wa Roho wa Mungu. Si mokosa kuwa tajiri, lakini ni makosa kupenda pesa. Si makosa kuwa maskini, lakini ni makosa kuvuja fedha kwa vitu visivyo na maana. Ujumbe wa Bibilia ambao waendelea kila wakati kuhusu utunzaji bora wa fedha ni kuwa wa maarifa.

### Mauzo

Fanya mauzo ya biashara yako kwa kadiri uwezavyo,tafuta namna yakuongeza mauzo kwa mfano,matangazo ya zawadi,punguzo la bei na mambo yanayofanana na hayo(promotion).Ongeza idadi ya wateja kwa namna ya promotion na jitahidi kuwahudumia vizuri wateja ili uweze kukuza biashara na kupata wateja endelevu.

## MFUMO WA BIASHARA

Katika dunia hii, kuna mifumo mingi ya kufanya biashara ambayo ni mizuri sana na itakusaidai katika kuinua kiapato chako na kuboresha hali ya maisha.Mifumo hiyo ni kama vile:

1. Duka

2. Franchise-Wafanya biashara wakubwa ambao unaweza kutumia nembo za kibiashara zao Kwa makubaliano maalum na ikakuwesha kufanya biashara kama hiyo

-mfano cocacola

3 .Biashara Mtandao.

Hizi ni biashara ambazo unaweza kufanya kwa kuongeza idadi ya marafiki na kukuweza kupata kipato kikubwa kwa kutumia muda mdogo na matangazo yasiyo na gharama.

NB:- Unapotazama biashara hii inalipa sana hasa kama umeamua kufanya kazi kwa juhudi. Mfano wa biashara mtandao ni EDMARK PRODUCT, FOREVER LIVING, GENERAL D ,BFSUMA na TIANSHEE.

Mzunguko wake na mtaji wake ni :

- Wanaopenda
- Wananunua
- Kuelezea kwa shauku wengine

## IJUE BIASHARA YA MTANDAO (NETWORK MARKETING) NA FAIDA ZAKE.
## KONA YA MJASIRIAMALI NA EDMARK HEALTHY LIVING & FINANCIAL PROSPERITY

Network Marketing (Biashara mtandao) ni biashara inayofanyika kwa kuwaunga zaidi watu kusambaza na kuuza bidhaa za kampuni kama wasambazaji ambao hulipwa kulingana na utendaji kazi wa mtu binafsi. Aina hii ya biashara huwa na kampuni linalozalisha bidhaa Fulani na kuziuza kwa kutumia wasambazaji waliokubaliwa na kampuni, ambapo wasambazaji hulipwa kamisheni kulingana na mauzo, lakini pia kupata faida fulani(retail profit) katika bidhaa hizo anapoziuza kwa mtumiaji wa mwisho. Hivyo msambazaji (distributor) anapouza zaidi ndipo kampuni nalo linapouza zaidi na kupata faida. Mfano mzuri wa network marketing ni kama wauzaji wa laini za simu wanavyopatikana na jinsi wanavyolipwa wasambazaji.

Makampuni mengine huuza bidhaa za vyakula, tiba lishe, madawa ya meno, bidhaa za mitindo, vifaa vya vyombo vya umeme (accessories), urembo (cosmetics) bidhaa za arts na aina mbali

RAYMOND CHIMBUYA

mbali za bidhaa zinazozalishwa na makampuni mbali mbali. Mfano wa hayo makampuni yanayofanya biashara zake kwa njia ya mtandao (network) ni kama FOREVER LIVING, GNLD, SUMA INTERNATIONAL, GREEN WORLD NA Kampuni zuri sana toka Malaysia la EDMARK INTERNATIONAL. Haya makampuni yapo pia hapa nchini ni ya biashara mtandao.

## FAIDA ZA BIASHARA MTANDAO

Katika biashara mtandao, faida kubwa majawapo kubwa ni Uhuru wa kutumia muda. Wote tunajua kuwa katika maeneo mengi ya kazi huwa na ratiba ya kazi ambapo mwajiriwa hutakiwa kuwasili kazini na kuondoka kazini. Hivyo kulisimamia hilo vizuri kunakuwa na mahali pa kusaini, mfano daftari la mahudhurio la wafanyakazi. Hapo unakuwa unaongozwa na muda uliwekwa na mwenye ofisi au taasisi hiyo maana ndiye boss wako. Hivi sivyo katika biashara ya mtandao. Katika network marketing hakuna mahali unapotakiwa kuripoti na kusaini uwepo wako kazini, hakuna boss wa mwenzake, kila mtu ni boss. Kila kitu kinategemea kujitoa kwako mwenyewe katika ratiba yako mwenyewe. Watu wengi sana katika biashara hii, wateja wao ni wale watu wa karibu yao, kama vile ndugu, marafiki na watu wanaofanya nao kazi au kuwasiliana kwa njia yoyote ile. Hivyo basi unaweza kuuza bidhaa muda wowote na mahali popote bila kuathiriwa na ratiba maalumu (fixed time schedule).

Zaidi kwa kuzingatia ratiba yako, unaweza ukawa na muda mwingi wa kutosha kukaa na familia yako, hasa watoto wako badala ya kuwaachia mabinti wa kazi ambao hata malezi yao hayana uhakika ( house girls). Hili haliwi rahisi kwa mtu anayeongozwa na ratiba ya ofisi, ndio maana wengine hufanya kazi siku zote saba za juma

.

## UHURU BINAFSI.

Tafakari nama gani boss ambaye unawajibika kwake, unakuwa boss mwenyewe, unatengeneza mtandao wako mwenyewe, wewe ndiye mwenye maamuzi ya kwanza na ya mwisho, unaamua upate fedha kiasi gani na kwa wakati gani. Hivyo unakuwa na uhuru wako binafsi ambao utakusaidia kufanya shughuli zako zingine nyingi.

## FURSA KUBWA ZA MAFANIKIO

Watu wengi wamekuwa mamilionea kupitia network marketing/biashara mtandao. Kwa kujitambua, nidhamu katika biashara na fedha, mafunzo na mtazamo sahihi kila mtu anauwezo mkubwa wa kufanikiwa katika biashara mtandao. Hivyo basi ukitaka kufanikiwa kiuchumi kwa kupitia network marketing, ni wewe kuwa utambuzi binafsi, nidhamu katika biashara na mawazo chanya ya kufikia ngazi za juu zilizowekwa na kampuni husika kulingana na mauzo yako.

### FURSA ZA MAFUNZO BURE.

Namna ya mafunzo ni rahisi sana, wengi tunakuwa na matamanio kufanikiwa kimaisha, tunaweza tukawa na mitaji mikubwa au midogo, lakini tatizo ni namna ya kuendesha biashara yoyote, na hata pale tunapojaribu kuanzisha jambo ya kututoa kimaisha tunaishia kupata hasara, kupoteza mtaji na kuilisika. Katika network marketing,au biashara mtandao  mafunzo mbali mbali yahusuyo biashara ya mtandao, hutolewa bure ili msambazaji aweze kuimudu biashara

pale anapoamua kujiunga mayo. Mafunzo yanakuwezesha kujua zaidi kuhusu bidhaa zitolewazo na kampuni, mfumo wa masoko (market plan), namna ya kupata kamisheni, faida ya papo hapo

(retail profit), na mafunzo ya uongozi katika biashara. Hivyo uwezekano wa kufanikiwa zaidi unakuwa wa uhakika kwa msambazi yeyote

RAYMOND  CHIMBUYA

MPANGO RAHISI WA BIASHARA

Mfumo wa biashara mtandao ni rahisi Sana, hauhitaji ujuzi fulani maalumu au masomo Fulani mahususi ili kuweza kuifanya hii biashara. Haihitaji matangazo maalumu kutangaza bidhaa zako, wasambazaji ndio huitangaza kwa kutumia midomo yao wanaponadi bidhaa lakini pia kutokana na ubora wa bidhaa, walio nunua huwa mabalozi kwa engine na hivyo kufahamisha na kujulisha zaidi uwepo wa bidhaa hizo sokoni. Aidha hutolewa vipeperushi, vitabum DVD na CD na aina zingine za maandishi kuelezea bidhaa, hivyo msambazaji au mtu yeyote anayekuwa katika biashara hii huokoa kiasi kikubwa cha fedha ambacho kingetumika kwa ajili ya matangazo mbali mbali mbali.

## KUFANYA BIASHARA UKIWA NYUMBANI/WORK AT HOME

Biashara hii haihitaji eneo fulani maalumu la kufanyia biashara. Mtu anaweza kufanya biashara hata akiwa nyumbani, maadamu tu anaweza kutumia internet, simu au kifaa chichote cha mawasiliano. Ni rahisi sana, kazi yako ni kuuza maneno, yaani wajulishe wengine uuze bidhaa zako. Huu ndio upekee na urahisi wa biashara ya mtandao ukilinganisha na biashara zingine. Zinawafikia watu wengi kwa muda mfupi. Unaongea kwenye simu na wateja wako na mahitaji yao. Whatsapp, email, Facebook, twitter, YouTube instagram, telegram na aina zingine za mawasiliano, watu wengi hupata taarifa za bidhaa zako kwa muda mfupi lkn wewe ukiwa tu nyumbani na hivyo kuuza bidhaa kabla hata hujaonana na mteja.

## KUTOKUWA NA MIPAKA NA JINSI YA KUIENDESHA

Biashara mtandao haina mipaka kutokana na njia zake zinazotumika kuuza bidhaa. Mipaka ya mataifa, na kijiografia inaondoshwa katika biashara hii. Haina gharama za kuajiri wafanyakazi

wengi ofisini na kukodi fremu za kuuzia. Mtaji wake ni Mdogo sana kuweza kuingia katika hii biashara ukilinganisha na biashara zingine nje ya mfumo huu. Kumbuka unaweza kuifanya na kuisimamia hii biashara hata ukiwa nyumbani kwako.

## KUPATA MSHAHARA/KIPATO CHA ZIADA

(Getting passive salary).

Faida na sifa nyingine ya kipekee ya biashara hii ya mtandao ni kuweza kupata kipato kingine cha ziada mbali na kile upatacho katika uajiriwa wako. Unaendelea kufanya kazi yako ya kila siku na kupata stahiki zako kama kawaida huku ukiwa nako unaingiza kipato kingine bila kuathiri kazi yako. Kumbuka hii biashara hufanyika mahali popote na muda wowote. Wengine hupata kipato kikubwa zaidi ya kile wanachikipata katika mishahara yao ya kawaida. Hilo

huwafanya wengine kufikia hatua ya kuacha kazi zao rasmi na kuisimamia biashara yao ya mtandao.

## KUENDELEA KUPATA KAMISHENI HATA KAMA UTASIMAMA KWA MUDA KUSAMBAZA BIDHAA.

Biashara ya mtandao ni ya kuunganishana, kutengeneza kama mnyororo ambapo anayekuunganisha anapata kamisheni ya point za kuunganisha distributor mwingine, mauzo yake binafsi na mauzo ya watu aliowaunganisha. Kwahiyo the more you join the others the more you get more commission! Hivyo unaweza ukaumwa usipate kuuza bidhaa zako, lakini wale uliowaunganisha wakiuza kwa upande wao, wewe pia unapata points za kamisheni kutoka katika

mauzo yao. Na unapiwaunganisha zaidi na kuuza ndipo cheo chako katika mtandao kinapandishwa na malipo yako kuwa makubwa zaidi.

## NI BIASHARA YA MILELE

Sifa nyingine ya biashara ya mtandao, ni kwamba ni ya milele. Ukijiunga na hii biashara unaweza kuendelea nayo maisha yako yote kwa angalau kununua bidhaa mara moja kwa mwaka mzima. Biashara hii kwa kampuni fulani nilijualo hurishishwa hata kwa watu walio nyuma yako, ikitokea maisha yako au uwezo wako wa kuendelea nayo umefika, basi utamrithisha mrithi wako kuendelea nayo. Hivyo uwezekano wa kuipoteza biashara hii au kufilisika ni mdogo sana ikifanywa kwa nidhamu na malengo.

Kwa leo ningependa nikomee hapa maana faida ni nyingi sana, zikiwemo za kusafirishwa nje ya nchi, tours za hapa na pale na mambo mengine yanayojili katika biashara mtandao. Aidha nitoe rai, si makampuni yote yanayofanya network marketing au biashara mtandao, ni bora na kwamba yanaweza kukutoa kimaisha. Wengi bila kufanya tafiti za kina kuhusu ubora wa kampuni, bidhaa zake na mfumo wa malipo yao, wamejikuta wanaingia kwenye hii biashara kwa kuambiwa kuwa inalipa pesa nyingi kwa muda mfupi, lakini hata hivyo mwisho walipojiunga wanajikuta wanabaki na bidhaa ndani, hawapati wateja na kupoteza fedha zao bure. Mfano mengine hadi

ufikie mauzo ya point kadhaa ndipo ulipwe, wakati mengine hata point moja unalipwa. Hivyo

RAYMOND CHIMBUYA

umakini mkubwa unahitajika kujiunga na hizi biashara za mtandao.

Kwa kuijua zaidi na ushauri kuhusu kujiunga na biashara ya mtandao (network marketing), tunaweza kuwasiliana kwa namba ntakazo hizo hapo chini.

NB: BIASHARA HII HAIHITAJI UCHOYO, UNAPOJIUNGA HAKIKISHA UNAMSAIDIA NA MWENZAKO KUWEZA KUJIUNGA ILI KUFANIKIWA KWA PAMOJA NA KUUSHINDA UMASIKINI. Remember PEOPLE HELPING PEOPLE SUCCEED.

**Ukipenda biashara hii, wasiliana name: RAYMOND CHIMBUYA (raymondchimbuya1977@gmail.com) 0755 14 88 97/0786 393 603/ 0655 14 88 97**

## KANUNI AMBAZO ZITAKUSAIDIA KUANZA NA KUKUZA BIASHARA YAKO KWA KUWA NA MTAJI MDOGO

Siyo lazima uwe na pesa nyingi ndipo uanze biashara, hapana mtaji mdogo utakuwezesha kufika kuwa na mtaji mkubwa kama utazingatia yafuatayo.

### Jipe muda, biashara haitaweza kukua kwa haraka

Kila jambo lina utaratibu, Musa hakuanza safari ya kwenda kuwatoa Waisrael kule Misri mara moja, alijifunza kwanza na kukuka kwa kwa kuhani Yethro, ndipo baaba ya kuwa ameiva ndipo

akaanza kumsumbua Farao kuondoka utumwani. Au mtoto anaanza kwa hatua kwa hatua,anzaliwa ,anakuwa taratibu kisha anakuwa mtu mzima ,anakuwa baba au mama,Hivyo hivyo biashara inaanza kukua taratibu mpaka inakuwa kubwa.Uzuri wa kuanza biashara na mtaji kidogo ni wazi kwamba kila mtu anaweza kuanza hivyo hivyo. Lakini pia urahisi huu wa kuanza biashara kwa mtaji mdogo unafanya ukuaji wa biashara kuwa wa taratibu taratibu,kama ilivyo madbadiliko ya maendeleo yanakuwa taratibu(Gradual change). Hivyo unapofanya biashara yoyote ambayo unaanza na mtaji mdogo ni muhimu ukajipnaga na kujiweke muda wa kutosha ili kuweza kukuza mtaji wako. Usiwe na tamaa ya kutaka kukuza biashara hii haraka, unaweza kuingia kwenye maamuzi ambayo yatakugharimu zaidi. Endelea kufanya biashara yako huku ukijifunza zaidi na kuangalia kila fursa ambayo unaweza kuitumia kukuza biashara yako ikijifunza mbinu mbalimbali toka kwa marafiki zako au mitandao ya kijamii pia na kwa wale waliofanikiwa.

## 2. Hifadhi au weka akiba wa mtaji wako taratibu

Usitumiye kupita kiasi ,kumbuka kuwewka akiba.Kwa kuwa mtaji wako ni mdogo ambao umeanza nao katika biashara yako,songa mbele jitahidi kuendeleza na kukuza mbinu mbalimbali za mtaji wako kila inavyoitwa leo,fikiri tofauti na jana,kila siku tafuta wazo jipya la kuboresha biashara yako,uwe na nidhamu katika biashara,marafiki na biashara ni vitu

RAYMOND CHIMBUYA

tofauti,epuka kuwaruhusu marafiki kuingilia katika bishara,mfano anachukua bidhaa bila kulipa ,eti kwa sababu ni rafiki yako.Hapana biashara inajitegemea na rafiki ni wa kwako. Endelea kuukuza kila siku. Usiendeshe biashara kwa kula kila kipato unachopata, badala yake tenga sehemu ya akiba irudi kwenye biashara yako. Fanya hivi kwa nidhamu ya hali ya juu sana na

Unahakikisha kila unapopata faida sehemu inarudi kwenye biashara yako. Pia endelea kuangalia kwa mazingira uliyonayo na kwa biashara unayofanya ni kwa jinsi gani unaweza kukuza mtaji wako zaidi. Kama utafikiria hili kila siku, utapata majibu chanya ya biashara yako.

## 3. Angalia gharama za matumizi yako

Usitumiye fedha katika matumizin yasiyo ya lazima.matumizi yako yaendane na hali yako ya kipato,siyo kwa sababu ni mfanyabiashara ,basi unatumia kiwango cha juu ambacho bado haujafaikia,utakapofikia kiwango cha juu,utatumia tu.Lakini mwanzo ni vizuri kurekebisha gharama za matumizi katika maisha ya kila siku.Hapa unahitaji kuwa mwanagilfu sana,mfano unachukuwa mchele kila moja na sukari kwa matumizi binafsi.katika kilo moj ya sukari na mchele ,labla faida ni shilingoi mia tatu,na kilo kilo i=unauza shilingi elfu mbili,kwa hiyo utakuwa umechukuwa faida ya kilo sita ambazo utakuwa umeuza kwa siku ngapi,hapa ni wazi kwamba umekula faida ambayo bado haujaipata.Matokeo yake ni nini,umekula mtaji au umekula siku ambazo haujaingiza faida.Kuwa kwenye biashara haimaanishi kwamba ndio una uhuru wa kufanya chochote unachotaka na fedha za biashara hiyo, kwa sababu tu ni zako. Wewe sasa upo kwenye wakati mgumu wa kukuza biashara yako huku ukiwa hauna njia nyingi za kufanya hivyo. Hebu kwa sasa punguza kabisa gharama zako za kibiashara na za maisha. Kama kitu sio muhimu sana basi usikigharamie. Punguza matumizi yote ambayo ni ya anasa tu na sio kwa ukuaji wa biashara. Katika kupunguza gharama zako za biashara na maisha, Jijengee nidhamu nzuri sana ya fedha. Usitumie fedha kiholela tu, kuwa na mahesabu na sababu kwa nini umetumia fedha fulani, hasa kwa matumizi ambayo sio ya kawaida.Fanya hivyo kwa faida ya

RAYMOND CHIMBUYA

kukuza biashara yako ***daima usije ukaanza visingizio visivyo na tija,mara ohoo,mapito,ohoo mashambulizi,ohoo,mapepo kumbe ni mashambulizio yako mwenyewe.***

## 4. Chagua marafiki

Kuna aina tofauti tofauti za watu.Wapo ambao kazi yao ni kukukatisha tama mara zote,hawawezi kukutia moyo,marafiki wa aina hii epukana nao kabisa,wapende kwa mbali usiwashirikishe katika mambo ya mafanikio y a biashara yako.Wapo marafiki wapenda maendeleo ,hao ni wa kushikiana nao tena ni wa kuambatana nao.Baada ya kuiendesha biashara

yako vizuri na ukaona inaenda kwa faida, unaweza kuangalia watu ambao unaweza kushirikiana nao kwenye biashara hiyo. Kuna watu wengi ambao wanaweza kuwa na mtaji lakini hawana muda wa kufanya biashara. Lakini pia watu hawa wanataka mtu ambaye wanaweza

Kumwamini. Hivyo kama unaweza kuaminika angalia watu unaoweza kushirikiana nao kibiashara. Andaa mpango mzuri ambao utamshawishi mtu ni jinsi gani yeye atafaidika kama atawekeza kiasi kidogo kwenye biashara yako. Ikiwa unaendesha biashara yako kitaalamu itakuwa rahisi zaidi kushawishi watu kushirikiana na wewe.Tunaposema kitaalamu ni vizuri biashara ukaisajili kwa maana kuwa na leseni na taratibu zinazokubalika katika sheria ya mahala husika,mfanosheriandogo(***ByLaws)auSheriakubwa(PrincipleLaws)***

## 5. Sajili biashara yako (Formalise)

Kuendesha biashara pasipo kurasimisha siyo vizuri, kwanza ni kinyume cha sheria lakini pia utakosa fursa ambazo zinaweza kukuza biashara yako.Hata kama biashara yako ni ndogo kiasi gani, irasimishe. Iendeshe kisheria kwa kuwa na namba ya mlipa kodi (TIN) na leseni. Kwa kufanya hivi biashara yako itakuwa katika nafasi mzuri ya mashindano na kukua na kuwa huru katika mashindano ya kibiashara.itakuwezesha kufahamika katika taasisi za kifedha pale utakapohitaji msaada zaidi wa kifedha. Mkopo kwenye taasisi za kifedha ni chanzo muhimu ila

RAYMOND CHIMBUYA

Usikimbilie kama bado hujaweza kuiendesha biashara yako kwa faida pia kumbuka hatutaka kopa bali tutakopesha. Hakikisha umeiweka biashara yako vizuri kwanza na inajiendesha kwa faida ili unapochukua mkopo unajua unauweka wapi na kuendelea kupata faida zaidi. Kuikuza biashara pale ambapo umeanza na mtaji mdogo ni kitu ambacho kinawezekana. Lakini unahitaji kujitoa na kujenga nidhamu kubwa. Unahitaji kufanya kazi zaidi ya wafanyabiashara wengine, unahitaji kuwa mbunifu wa hali ya juu na pia unahitaji kujijengea uaminifu. Ukishajua wewe biashara yako ni ndogo na inahitaji kukua, basi hakikisha kila mara unaumiza akili yako ifikirie

njia zaidi za kuikuza. Na kama utaweza kufanya hivi basi utaziona fursa nyingi zilizokuzunguka za kuikuza biashara yako daima.***Ubarikiwe Uwe na Moyo wenye ushupavu***.

## Biblia inasema nini kuhusu Mkristo kuingia katika madeni? Ni makosa kukopa au kukopesha pesa?"

Jibu: Maneno ya Paulo kwetu katika Warumi 13:8 msiwe na mtu chochote bali kupendana kwa maana ampendaye mwenzake ametimiza sheria.tusiwe na lolote bali ile ya upendo ni ukumbusho wa nguvu wa chukizo la Mungu kwa aina yo yote ile ya deni ambazo hazijalibwa kwa wakati ufaao ( Zarubi 37: 21). Kwa wakati huo huo, Bibilia kabisa haiamrishi kinyume na aina zote za madeni. Bibilia inatuonya kuhusu madeni, na kutia moyo hali ya kutokuwa na madeni, lakini haikatazi madeni. Bibilia iko na maneno makali ya hukumu kwa wakopeshaji ambao wanawatusi

**Wale ambao wameshindwa kuwalipa, lakini haiwahukumu wenye deni.**

Watu wengine wanauliza juu ya riba ya mkopo wowote, lakini mara nyingi katika Bibilia tunaona kwamba riba ya kadri inatarajiwa kupokewa katika pesa ambazo zimekopwa (Methali 28:8; Mathayo 25:27). Katika Israeli ya zamani sheria haikukataa kutoza riba katika viwango vya mkopo-zilizopeanwa kwa maskini (Mambo Ya Walawi 25:35-38). Hii sheria ilikuwa na maana

katika maisha ya, kawaida, kifedha, na kiroho, lakini mbili ndizo za maana kutajwa. Kwanza, sheria kwa kweli iliwazaidia maskini kufanya hali yao isiwe mbaya. Ingekuwa vipaya kuingia katika umasikini na ingekuwa jambo la kuaibisha kutafuta usaidizi. Lakini ikiwa juu ya kulipa mkopo, mtu maskini aliitajika kulipa riba, jukumu ambalo lilikuwa la kufedhehesha sana kuliko.

Pili, sheria ilifunza somo la maana sana kiroho. Kwa mkopeshaji kutolipisha riba kwa mkopo kwa mtu lingekuwa tendo la ukarimu. Atapoteza hizo pesa zilipokuwa kwa mikono mingine. Vile vile hiyo itakuwa njia ya ushahidi ya kudhihirisha shukrani kwa Mungu kwa huruma zake

ambazo halipishi watu wake kama “riba” kwa neema ambayo ameifikisha kwao. Kama vile Mungu kwa huruma zake aliwatoa Waisraeli katika Misri wakati hawakuwa kitu cho chote na kuwa watumwa alikwisha wapa nchi ambayo ni yao (Mambo Ya Walawi 25:38), kwa hivyo aliwatarajia waonyeshe ukarimu huo huo kwa raia wenzao maskini.

Wakristo wako katika hali sambamba kama hiyo. Maisha, kifo na kufufuka kwa Yesu kumetulipia deni ya dhambi zetu kwa Mungu. Sasa, vile tunapokuwa na nafasi tuwazaidie wengine, hasa wale ambao ni Wakristo, kwa mikopo ambazo haziwezi ongeza shida zao. Yesu hata alitoa mfano unayohusiana na mambo haya kuhusu wadeni wawili na nia yao juu ya kusamehe (Mathayo 18:23-35).

Bibilia vile vile haikatazi au kuhukumu kukopesha pesa. Hekima ya Bibilia yatufunza kwamba kila mara si hoja nzuri kuingia katika deni. Deni hasa hutufanya kuwa mtumwa kwa yule anayetupa mkopo. Kwa wakati huo huo, katika hali zingine kuingia katika deni “dhambi ya lazima.” Vile pesa zinavyo tunzwa kwa hekima na malipo ya madeni yamedhibitiwa, Mkristo anaweza kuchukua mzigo wa deni ya kifedha kama hiyo italazimu.

Ujasiriamali KWA Maendeleo Endelevu.

# HEKIMA YA KI-MUNGU KATIAK MAFANIKIO

(Mafanikio 3Yohana 1:2)

**Kanuni:** Nguvu za Kiroho (saidia wajane)---MITHALI 19:17

: Nguvu za kiakili----kutoka 31:1-11

: Nguvu za kimwili-----kutoka 23:25-27

Hautakuwa na magonjwa

Utaishi kwa mpango wa Mungu

Utaogopwa/Utisho

: Kusikia sauti ya Mungu---28:31-39

: Kutokata tama

: Kushika neno---Zab 89:34-35

: Wivu wa maenedeleo

: Kutenda mema---1petro 2; 15/ kuishi katika kweli (2yohana 1:4)

Maana ya biashara:-

Ni shughuli yeyote inayofanywa kwa lengo la kupata faida(vigezo, faida, halali)

Maana ya ujasiriamali:- Ni mchakato wa kutambua fursa, kuzitumia na kuanzisha shughuli za kijamii, za kiuchumi na Taifa.

Hatua za ujasiriamali:

(a) Ugunduzi

(b) Ubunifu na wazo la biashara

(c) Kuwa na mpango wa biashara

(d) Utekelezaji

(e) Tathmini.

## SIFA ZA MFANYABIASHARA:

(1) Kufuatilia mwenendo wa bei

(2) Kutambua ugavi na utashi pia hujua ni kiasi gani kinahitajika na kuzalishwa.

(3) Kuwa na uhakika wa huduma kwa mteja, hutoa bei nzuri kwa mteja na kujaribu kuwasaidia wazalishaji wake.

(4) Hukusanya taarifa za mwenendo wa wateja

(5) Hupokea haraka mrejesho na ufanisi

(6) Husukumwa na mafanikio na anakuwa msaada hata katika mazingira mapya

(7) Huuza na kununua wakati wote.

## MAMBO YA KUZINGATIA:

i) Kutambua wateja

ii) Kutambua vizuri ukubwa wa eneo ambalo wateja wanapatikana

ii) iii) Kufahamu mahitaji ya wateja

iv) Kufahamu wauzaji waliopo

RAYMOND CHIMBUYA

## NAMNA YA KUTAMBUA WATEJA:

- Akina nani
- Wanafanya nini
- Wananunua wakati gani
- Wanategemea nini
- Wanafikiria nini kuhusu washindani wako
- Wanatarajia kupata huduma gani kutoka kwako

## UWEZO WA KUSIMAMIA BIASHARA:

Kupanga gharama za biashara (COSTING)

Kukokotoa kiasi cha fedha ulicho tumia katika kununua bidhaa katika biashara yako

AINA ZA GHARAMA:

Gharama za moja kwa moja

Gharama zisizo za moja kwa moja

## MANUFAA YA KUFAHAMU GHARAMA ZA BIASHARA:

Kupanga bei

Kufahamu kama unapata faida au hasara

Kufahamu vitu vinavyo kugharimu sana katika uendeshaji wa biashara yako

RAYMOND CHIMBUYA

MASOKO:

o Ni wateja au wanunuzi wa bidhaa zako

o Ni shughuli zote zinazo fanyika katika kuongeza mauzo

o Ni jinsi ya kuwaridhisha wateja na kutengeneza faida kwa kuwaletea bidhaa au huduma wanayo hitaji.

KUONGEZA MAUZO:

Bidhaa

Bei

Banda/duka/eneo la kufanyia biashara

Bango

KUMJALI MTEJA:

Hamasa

Kubali kukataliwa na mteja katika mchakato wa kuuza

Mhudumie mteja kwa wakati

Kuwa mpole na mkarimu

Kuwa mvumilivu

Toa msaada na huduma bila malipo wakati wote

Kuwa mnadhifu wakati wote

## MAKATAZO:

Usibishane na wateja

Usiwachangane wateja na bidhaa nyingi kwa wakati mmoja

Usimlazimishe mteja kununua kitu asichokitaka

Usikate tama

Usinywe ,usile wala kuvuta wakati wa kumhudumia mteja

Chaoooooooo, chuchuuuu/ mambo hayo.



RAYMOND CHIMBUYA

## WASIFU WA MWANDISHI

**Raymond chimbuya anafanya kazi katika kada ya utawala,amefanya kazi hii kwa muda mrefu .Katika shughuli zake za kila siku anashughulikia sana kutatua matatizo mbalimbali ya jamii,mara kadhaa anafanya utafiti wa matatizo mbalimbali yanayosumbua katika maisha ya kila siku ya kiuchum**

**Amepata uzoefu mkubwa katika masuala ya ujasilia Mali, kutokana Na ustadi huo, ndiyo sababu ameamua kuandika kitabu hiki ili kuweza kuponya uchumi kwa muktaza wa Hekima ya Mungu.**

**Raymond chimbuya ni mwanamapinduzi anayetarajia kuandika vitabu vingi katika kuelimisha jamii.MUNGU AKUBARIKI.**

**Mwandishi ana shahada ya Uzamili, Shahada ya Theolojia Na Maendeleo ya Jamii, shahada ya Sheria, Shahada ya Sayansi ya Jamii na Cheti cha Elimu ya Biblia.**

